*République Démocratique du Congo*

**MINISTERE DE L'ENVIRONNEMENT, CONSERVATION DE LA NATURE ET TOURISME**

---

**DIRECTION DES INVENTAIRES ET AMENAGEMENT FORESTIERS (DIAF)**

# Kitabu Cha Haki Na Sharti Za Shirika Zote Zinazo Elekewa

*Mwezi wa sita 2010*

# DAFTARI

I. UFUNGUO ........ 3

II. SHERIA YA UDONGO NA SHERIA YA MSITU ........ 5

II.1. Umbo Ya Haki Ya Udongo Ya Shirika La Wakaaji Mahali ........ 6

II.2. Upana Wa Anga, Wa Milki Ya Shirika La Wakaaji Mahali ........ 7

II.3. Kuto Kunyanganywa Kwa Udongo ........ 8

II.4. Haki Binafsi Katika Milki Ya Udongo ........ 8

II.5. Uwezo Wa Kustarehe Na Milki Za Udongo Za Shirika La Mahali ........ 10

II.5.1. Wazo la kwanza ........ 13

II.5.2. Wazo la pili ........ 14

II.5.3. Wazo la tatu ........ 14

II.6. Sheria Ya Udongo Na Milki Za Udongo Za Shirika La Mahali ........ 14

II.7. Misitu Za Asilia Wakati Wa Utawala Wa Wakoloni ........ 15

II.8. Yanayo Husu Sheria 011-2002 Ya Tarehe 29 Agosti 2002 Juu Ya Sheria Ya Msitu (Code Forestier De 2002) ........ 16

II.9. Kujulisha Mahali Ya Shirika Za Wakaaji Mahali Katika Mgao Wa Udongo ........ 19

II.10. Misitu Na Haki Za Matumizi Za Wakaaji ........ 20

II.11. Kinyume Cha Mabadiliko Ya Barua Ya Makusudiyo Ao Ya Kudhamini Kuweka Akiba Katika Eneo La Msitu ........ 22

II.12. Mgao Wa Inchi Na Misitu ........ 24

III. KIFUPI CHA HAKI NA SHARTI ZA SHIRIKA MBELE YA MATUMIZI YA MANUFAA YA MSITU ........ 27

III.1. Katiba Na Mipango Ya Matumizi ........ 27

III.2. Haki Na Sharti Za Shirika Mbele Ya Matumizi Ya Manufaa Ya Msitu ........ 28

III.3. Serikali, Mwenyeji Manufaa ........ 29

III.4. Wapewaji Eneo Za Msitu ........ 31

III.5. Wakaaji Na Shirika Mahali ........................................................................ 34

IV. KWA MWISHO ........................................................................................ 36

V. VITABU VILIVYO TUMIWA........................................................................ 37

V.1. Niaraka halali ........................................................................................ 37

V.2. Vitabu Ao Maandiko Mbalimbali............................................................. 38

*Hizi buku zili andikua na mwalimu Kalambay Lumpungu, wa Darasa la sheria ya masomo ma kuu ya Kinshasa, kwa shabaa ya ku onesha somo la kwanza kwa vikundi, matumikisho ya udondo na mazao ya pori. Zili oneshwa na ku hakikishwa na kamati ndongo iliyo undua. Chini ya uongozi wa chumba cha hesabu na matengenezo za pori (DIAF) ya chumba cha waziri wa mazingira Akiba na Matembezi.*

# I. UFUNGUO

Katika hali zinazo angalia funzo ya vikundi mbalimbali vilivyo egemea upande unao angalia sheria ya msitu (Code Forestier) ya 2002 na nyaraka ya matumikisho, chumba cha Waziri kinacho husika na mazingira, akiba la umbo na matembezi ina nia ya kuandika kitabu moja juu ya haki na sharti ya watu wote watakao yatumikisha. Kuandikwa kwa kitabu hiki ni kwa lazima saana, kufanana na tafsiri nyingi za wasomaji na pia umbalimbali kati ya haki mpia na haki ya mazoezo na ya namna ya kuona kwa wenye haki juu ya msingi, unaleta kukosa masikilizano katika malumbano na ni misingi ya magonvi mengi. Kwa haya, kunaongezwa masemi ya watu fulani wanao tumika nao pamoja, kwa ajili ya maendeleo wanayo pana tafsiri zao za nyaraka. Haya yanatoka kufuatana na habari zisizo faa, zisio heshimu maana ya katiba na sheria zingine.

Katika matumikisho ya sheria ya msitu na ya nyaraka zake za matumikisho, uhakimu wa msitu utafanya ujuvi na mapatano na vikundi vya wakaaji wa nafasi kwa misingi mbalimbali, kama vile:

- Kutia mipaka eno la msitu kwa kufanya mgao wa msitu;
- Mapatano kwa mambo yanayo angalia ushiriki ulio katika buku la mahitaji;
- Kutia mipango ya matengenezo juu ya msitu ulio pangwa, eneo la msitu na nyingine;
- Kutimiza upekuzi wa ushirika na uchumi.

Kazi kama hizi zinatimizwa baadae wakaaji wa julishwe vizuri juu waweze zungumza juu ya mambo yenye wanaelewa. Kwa hiyo, uhakimu wa msitu haupashwe kuacha nafasi kwa udongo, kwa kukosa habari, kwa mambo kufanyika kwa nguvu ao kwa habari isiyo kamili ndani ya mambo haya ya muhimu. Ina ombwa mbele ya yote kutia nukta ya juu ya haki na sharti ya vikundi vyote vya lazima ndani ya mambo haya kutumia eneo la msitu. Ni ya muhimu offisi ipane habari ya waziwazi na inayo enea juu ya msingi huu na yote inayo ombwa kwa kuyatimiza, na ipane namna ya mafanizio na namna ya kuepuka kukosa masikilizano ndani ya malumbano uhakikisho inapashwa andikwa ndani ya kitabu kinacho geuzwa katika lugha ya taifa na kupelelezwa zaidi kwa wakaaji mbele ya kuanzisha ujuvi wowote. Habari ita ruhusu vilevile kwa vikundi vyenyi kuelekewa, waelewe vizuri mambo yote na wajue haki na mapashwa ya kila mmoja, wakiepuka kwa kuya hepuka hiyi magonvi mengi.

Habari hii inatolewa ya kwanza kwa wakaaji wa nafasi ili wajue waziwazi sheria ya msitu pia vilevile haki na sharti zao. Itakuwa vilevile ya muhimu saana kwa wajumbe wa majimbo wa offisi, wa viwanda vya vifaa msitu, kwa wajuvi, shirika zisizo kuwa za kiserikali, na wafanya kazi wengi watakutana na mabishano juu ya haki ya aslili, haki ya kutumia na haki juu ya udongo.

Haki ni mchangano wa kanuni zilio kuwa sharti yenye kuongoza maisha kati ya watu. Kanuni inayo onyesha haki zenye watu wanaweza jipikia kifua na sharti zenye wanapashwa heshimu mbele ya watu wengine.

Kwa kweli usawa wa shirika inaomba kanuni zenye zinaongoza matendo ya wanamemba wake, na bila uhaki yenye inaleta ndani ya shirika heshima ya kanuni, ina leta usawa.

Mbele ya kufika kwa wajumbe wa Ulaya, shirika ya asili ya Kongo ilikuwa asili, sheria na namna ya uhamzi. Sheria hiyo ina itwa ya asili, ina tofauti kufuatana na vikundi vya kabila, kabila na vikoo vilivio na shabaa ya kukinga faida yao daima. Sheria ya asili inamo mitawi yote ya sheria iliyo kuwa ya muhimu kwa maisha ya ukoo, sheria ya siasa na uhakimu, sheria haki za watu na magawaniko yake (haki ya watu, ya vitu kwa upekee sheria ya udongo na sheria ya sharti), sheria ya ku azibu mipangiliyo uamzi na mwenendo. Mbele ya kuundwa kwa inchi huru ya Kongo, kwa kutawala udongo, wazungu wa Ulaya walifanya mikataba juu ya udongo na viongozi wa ma kabila na wa vizazi. Serikali huru ya Kongo wali heshimu mikataba hiyo ndani ya sheria yake.

Kwa njia ya sheria ya ufalme ya tarehe 29 Mei 1885, mfalme Leopold II alitangaza kuwapo kwa inchi huru ya Kongo na tarehe 01 Agosti ya mwaka ule, aliandikia kwa kujulisha inchi iliyo na uwezo, zilizo shiriki ndani ya mkutano wa Berlin kama yote ilikuwa ya shirika ya mataifa ya Kongo inakuwa tangu leo inchi huru ya Kongo. Ndani ya Afrika, kiongozi mkuu kwa njia ya kibarua chake cha vivi cha tarehe 01 Julai 1885, anajulisha yeye pia wote wasiokuwa wakaaji wa asili walio patikana ndani ya Kongo, kutangazwa kwa katiba ya inchi chini ya mamlaka ya mfalme Leopold II. Siku ile moja, kiongozi mkuu alitia saini sheria mbili yenyi moja yao inaangalia kutawaliwa kwa udongo.

Moja ya huzuni ya kwanza ya serikali, inchi huru ya Kongo ilikuwa ya kukanunisha mambo ya udongo. Ndio maana sheria ya tarehe 01 Julai 1885 na sheria zingine zilizo fuata ziliwekwa kwa heshima ya sheria ya udongo ya Kongo mpaka siku ya kutangazwa kwa sheria ya tarehe 20 Julai 1973 inayo angalia sheria kuu ya vitu, sheria ya udongo na vitu visivyo hamishwa na sheria ya ukingo.

Amri ya 1 cha sheria ya tarehe 02 Julai 1885 na amri pili ya sheria ya Waziri cha tarehe 14 Septemba 1886 inatangaza kanuni ya heshima ya haki ya kutawala kwa wakaaji wa nafasi ao wa asili. Kuona yote yenyi kupatikana kwa leo ndani ya vikundi vya wakaaji wa nafasi juu ya matumizi ya udongo na ya msitu, ni ya muhimu kujulisha tena kwa vikundi vyote vinavyo elekewa kanuni ya asili zinazo ongoza mambo ya udongo na ya msitu.

Kitabu hiki kinaoneshwa kwa sehemu mbili; sehemu ya kwanza inasema juu ya yote inayo angalia sheria ya udongo na ya sheria ya msitu, na sehemu ya pili juu ya haki ya vikundi mbele ya matumizi na juu ya matumizi ya manufaa ya msitu.

## II. SHERIA YA UDONGO NA SHERIA YA MSITU

Haiwezekane, kwa kujifunza sheria fulani, kuachanisha maneno yenyi kuongoza shirika, kwani kila chumba, hata ndani ya shirika yenyi haina mipangiliyo, ina philizophia ya upekee yenye ina ya ruhusu usikivu wa akili na unao eneo la shirika wanao taka. Kufuatana na usikivu wa sheria ya udongo ya asili, shirika nyingi inayo elekewa, wanaifanya si juu yao wenyewe lakini ni kufatana ao kulinganisha na sheria ya inchi za ulaya. Kwa maneno haya, H.LEVY-Bruhl alikuwa anashauri wakati ule kwa mwaka 1956 ndani ya maandiko yake yaliyo itwa «Maingiliyo kwa mafunzo ya sheria ya asilia ya wa Afrika», iliyo andikwa ndani ya kitabu cha mataifa ya sheria ya kulinganishwa no 1-ukurasa 67-77, kwa wote wenye vutia kwa majifunzo ya watu bila maandiko waache kutafuta kuwakaza watumikie usikivu wao wa maneno na mulindo wao wa kuwaza, lakini ni wazi ingie ndani ya hali watu hawa wanao kaa.

Shauri hii ina niya ya kweli kwani kishina ya mafanyizio ao ya kutumia udongo wa ki asili inapatikana ndani ya kanuni ya mpangiliyo wa shirika na siasa, kwani mpangiliyo wa shirika, wa siasa na sheria ya udongo ina ungana na ina shabaa moja: kukaza umoja na udaima wa vikundi. Kukosa kujua zaidi ya mambo haya, inapashwa tu kuleta upotevu ndani ya namna ya kuona yenyi Emile POSSOZ aliita «KIZUNGU».

Tuta onyesha kwa mistari inayo fuata, ya kwanza, haki amri ya watu wote na vikundi vya wakaaji wa nafasi na ya kufuata haki za upekee ndani ya mali ya watu wote. Mchango wa vikundi vya wakaaji wa nafasi wana patikana ndani ya mahali ya watu wote, chefferi, na mchangano wa vijiji, na vijiji, kufuatana na sheria ya ndani

no 08-016 ya Octoba 07 2008 juu ya muundo, mpangiliyo na matumikiyo ya sehemu zote za inchi ziliyo pewa mamlaka na ripoti yao, na serikali pia na majimbo.

### *II.1. Umbo Ya Haki Ya Udongo Ya Shirika La Wakaaji Mahali*

Ginsi itaonekana kwa mbele, kikundi chote cha wakaaji wa nafasi kina udongo wake. Udongo huu ni haki yake kwanza na pia ni haki ya watu wote kwa maana ni ya wakaaji wote wa asili wanao kuwa kundi la watu mbalimbali wenye hawawezi fasiriwa, wenyi kueneza sharti moja zenyi ziliwekwa na asili. Kanuni ya sheria ya nafasi ya watu wote hii ni kusema haki juu ya udongo zina changiwa na watu wote, ni kusema haki hizo zina gawanywa wakati nyingi kati ya watu wote, kwa watu wenye kupatikana, kwa kundi ya watu hawa, kwa maana kila mtu ana haki ya kutumia udongo, kama vile kikundi kina haki ya kutia namna na mipaka ya matumizi kwa watu wengine na kwa kila mtu. Ni ya muhimu kujua juu ya nukta ya hii kama sheria ya asilia haiko juu ya mtu moja: faida ya upekee inapashwa kuvutwa mbele ya faida ya watu wote. Nakwa hiyo hesmi upeke zaidi. Sheria ya asili haiko ya kikundi, sababu kama kuna vitu na kazi ya watu wote, sharti ya ushirika, haki za kila mtu zinabaki nyingi.

Ivi, kikundi kilicho cha asili ni mwenyeji wa haki ya amri inayo enda njia moja na milki yake ya udongo. Haki yenye kutumiwa na kikundi na wanamemba wake njia moja juu ya milki ya udongo hazi elewane vizuri na hazi linganishwe na haki ya inchi ya magharibi inchi za ulaya.

Kikundi cha wakaaji wa nafasi ni mwenye haki ya mamlaka ya watu wote juu ya udongo wake; kikundi hiki na wanamemba wake wanatumia juu ya udongo huo mchango wa chapa ya haki juu ya mzigo wa udongo unao umbo na vipimo mbalimbali.

Kwa kweli, kikundi cha asili kinacho toka iwe ndani ya vikundi vya jamaa, iwe ndani ya vikundi vya siasa, kwa njia ya mkubua wa udongo mwenyi anaweza kuwa vilevile kiongozi cha kikundi cha siasa, ana ustawishi na anaongoza matumizi ya milki ya udongo ya kikundi. Wanamemba wa kikundi hiki, kwa ngambo yao, wana haki kila moja ya kufurahia juu ya udongo. Haki hizo ni za upekee, ni kusema kama mtu mwenye kuishi ana haki ya kuchagua faida yote yenye udongo unamletea: mawindo, Uvuvi, mavuno ya mazao maumbile, na kadhalika, haikatazwe haki hizo zikanunishwe na mkubwa wa msitu ao kiongozi wa (mji) kijiji.

Hata hivyo, haki hizo za vikundi zina upekee wa muhimu kwani zina patikana kati ya haki za siasa na haki binafsi. Kwa kweli kutumikia haki ya kufurahia kwa

huru na ya kuenea iliyo kuwa ya kila mtu juu ya udongo wa kikundi fulani, ina weka. Mbele ya yote, kama mtu huyo ni mmoja wa kikundi hiki kipimo cha wenyeji udongo.

Namna ya kuwa mmoja wa kikundi ina kinyume juu ya umbo la haki ya upekee yenyi kila mtu moja anaweza kupata kwa faida yake mwenyewe juu ya udongo. Hali inapishana, ikiwa mtu huyo ni mwanamemba wa kikundi ao ni mgeni wa kikundi hiki, kwani kama ndani ya matumizi ya haki ya kutumia ya watu wote, hakuna tofauti kati ya mwanamemba wa kikundi , mwanamemba anae ingizwa na mgeni, tofauti hii ni ya ndani kwa yote inayo angalia haki ya upekee zinazo julikana kufwatana na umbo lake. Inafaa kujua kama haki ya kufurahia iliyo kuwa ya watu wote ina fatana na makao ndani ya kikundi.

### *II.2. Upana Wa Anga, Wa Milki Ya Shirika La Wakaaji Mahali*

Kuwekwa kwa udongo kunaweza kuwa na shina mbalimbali yenyi ina ungana na muundo wa kikundi. Mafunzo ya mpangiliyo ya siasa inapana mashina ya vikundi vya majamaa na vikundi vya siasa.

Kwa kanuni, kishina kia shirika ya kabila ni jamaa.

Mwanzo wa shirika ya kwanza inapatikana ndani ya mpango wa jamaa na upana wake. Ivi, udongo wa shirika hilo itakuwa kwa kinyume mchango wa udongo wa wanamemba wa jamaa hizo ao kabla ya jamaa hizo.

Aina ya vikundi vinavyo undwa juu ya jamaa si nyingi, ao hazipatikane ndani ya shirika ya wa Kongomani ya zamani, kwani ni kipindi cha kwanza cha maendeleo ya shirika ya mchango wa jamaa. Imeonekana kama mkusanyo wa jamaa nyingi, walijipa mpangilyo wa siasa, mikusanyo hiyo ili ungana kwa oda ya kugawa migawanyiko inayo kuwa chini ya mchango wa jamaa ndogo mchango wa jamaa na kabila. Aina ya michangano hizo ni nyingi pa Kongo.

Aina ya tatu, zenyi hazi onekane mara nyingi ni michangano ya siasa.

Ndani ya michangano inayo onekana ya siasa, kata ina udongo mbalimbali inayo pewa kwa kila moja ya vikundi. Kwa michangano hiyo, udongo na kata haina tofauti. Kwa michangano ya siasa, ni kata ndiyo inaonesha upana wa udongo.

Uchambuzi kwa upole unaonesha kama kishina cha sheria ya udongo kina panwa na vikundi vya vizazi na wasimamizi wa mgawanyiko wa siasa wasio kuwa na udongo wao, lakini wana tumikia tu uwezo wa siasa juu ya sehemu ambazo kwa wakati wote zinachanga njia nyingi ya udongo.

Kufuatana na hiyo inayo onekana, inawezekana kusema kwa mwisho kama kunapatikana umoja wa kanuni ya udongo ndani ya inchi yote ya Jamhuri ya Kidemocratia ya Kongo. Ivi ina wezekana kusema kwa aina mbili ya mchangano, haki ya kundi lote la wakaaji na wanamemba zina tiwa mipaka na upana wa udongo unao kuwa udongo wao wote, udongo wenye wakaaji wa nafasi fulani ni wenyeji udongo wa kila kikundi cha wakaaji wa nafasi unajulikana na kutiwa mipaka kwa namna njema.

Haki ya kikundi hai angalie tu undani lakini pia inaingizwa mpaka mwisho sawa vile kuni, miti, na kadhalika…

### *II.3. Kuto Kunyanganywa Kwa Udongo*

Kuto kunyanganywa kwa udongo kunatoka zaidi kwa hivi, udongo ni wa watu wote, hiyo inaonyesha kama mipaka ya udongo haiwezi badilika.

Kutokana na kutokunyanganywa na ya kuwa kikundi tu, kuna hali moja ya muhimu. Kwa kweli, ndani ya sheria yote ya msitu iliyo ya asilia, mgeni anaweza kupata haki ya kufurahai yote isiyo hamishwa kwa upekee, lakini inafaa ruhusa ya mwenye madaraka wa wakaaji wa nafasi. Kufurahia hiyo ina kinyume vilevile, sawa vile ile ilisemwa juu, kupata ruhusa ya kufurahia ya watu wote kinacho ungana na makao. Ni kufuatana na nia hii ndio inafaa kujua kama wakaaji wa nafasi wakati wa mbele ya mwaka 1885 walipatia wazungu wa Ulaya walio tia makao yao juu ya udongo wao haki ya yote isiyo wezekana kuamishiwa, iwe kwa wakati usio julikana mwisho, iwe kwa muda mfupi unao tiwa mipaka.

### *II.4. Haki Binafsi Katika Milki Ya Udongo*

Mtu moja anaweza kutumikisha katika milki ya msitu wa watu wote, hesabu fulani ya haki juu ya msitu, haki ya kutumikisha inayo ungana kwa uhakika na haki ya makao na haki za upekee juu ya udongo ambao shina ni kazi ya upekee zinazo ambatana na udongo.

Kufuatana na milki ya msitu ya kundi ya wakaaji wa nafasi, wanao uwezo kipekee wa kuweka makao yao, wanamemba wa wakaaji wa vikundi ambacho watu wengine wanaita wenye haki, lakini pia watu wanao ingizwa katika kikundi hiki cha wakaaji. Yanaweza kufanyika kwa njia ya ndowa ambayo muke anaishi katika kikoo cha mume wake ao unyumba ambamo mume anaishi katika kikoo cha muke wake, ao kwa njia ya kukubalia ulezi ao kwa mbinu zingine zote za mazoezo. Wageni wanaweza vilevile kukubaliwa kuishi katika udongo wa wakaaji wa nafasi. Kwa

mwisho, kwa kuona mambo yanayo angalia haki ya kipekee ina ambatana na kuwa moja wa kundi fulani, kwa upeo wa uaminifu katika kundi, wakaaji wote kila moja kufuatana na kimo cha upekee cha kila moja, hawana haki moja za kipekee.

Katika sheria ya asili, kwa kurizia haki ya vitu vilivyo imara, yafaa kukaa hakika katika udongo na kuyapa samani kwa njia ya kazi.

Na kwa hiyo katika kawaida ya mazoezo za msitu, hakuna wenyeji wa udongo wakubwa, kwa sababu kila mtu anakaa katika udongo kufuatana na mwisho wa nguvu wa mikono yake. Kwa hiyo, haiwezekane kuridhi udongo ambao hautaweza kuyapa samaani baadae.

Ikiwa haki ya wenyeji inazaliwa kwa njia ya kazi, inafutika vilevile kwa kukosa alama za kuyapa samaani ao ya makao. Juu ya neno hili uandishi wa haki ya vyote vilivyo imara yanaweza kubadirika kufuatana na mazoezi mbalimbali, Kwa ginsi ya makao ao elimu yaliyo kweli popote ni kusema kila mtu anapashwa kuonyesha kwa matendo, ao kimia ao kwa wazi, mapenzi utashi ya kuzimisha haki hizi. Kwa hiyo, sehemu ya udongo iliyo msingi wa haki za kipekee yanarudi katika mali ya kundi la wakaaji ambae waliyatoa.

Ikiwa ni kwa kufanya tayari kazi ya upekee, haki ya kuuza ao kuacha ni jumla kwa mwenyeji lakini haki hii inakuwa na mipaka wakati tendo la kukubaliwa linachanga pia vilevile kugeuza kwa udongo. Kwa hiyo, mazoezi inaleta tafauti ya kweli kati ya wenye kufaidika na tendo, kufuatana na ginsi wapo wana memba wa kikundi cha wakaaji wa nafasi wanao julikana, watu wanao ingizwa katika kikundi cha wakaaji wa nafasi ao kwa mwisho, wageni wa kikundi cha wakaaji wa nafasi.

Kwa watu wa aina ya kwanza, darage ya uaminifu inaweza kufanyika kati ya watu walio hai kwa ajili ya kifo bila ruhusa ya sultani ya udongo ao mji. Sababu ni sehemu ya kundi ya wakaaji wa nafasi.

Tendo la kuamisha linapashwa kukubaliwa na milki inayo uwezo ikiwa mufaidizi ni mgeni katika kundi la wakaaji wa nafasi.

Ikiwa watu wanao ingizwa katika kikundi cha wakaaji wa nafasi na wageni kwa kikundi hiki wana vilevile haki ya upekee juu ya udongo kwa kukaa kati na kuyapa samaani, haki hii, ni haki ya muda mfupi juu ya mali ya wakaaji wa nafasi wanayopokea. Muda wa haki hii yana ambatana na mambo mengi.

Kwa hiyo, kwa watu walio ingizwa katika kikundi cha wakaaji wa nafasi, haki ya yote yanayo kaa ya upekee itafuatana na mwendo wa vifungo vinavyo wachanga na kikundi cha wakaaji wa nafasi. Ni kwa hivyo, kwa njia ya ku vunja ndowa, mume

fulani ao muke fulani anaweza kupoteza haki yake kufuatana na ginsi moja kati yao alivyo ao hapana katika milki ya msitu isiyo ya yale kikundi cha wakaaji wao.

Sababu katika unyumba wa mazoezo, kanuni zinazo tumiwa kufuatana na makao ya wanaume ambayo inaweza kuwa ingine katika ukoo ao jamaa wa mume ao katika makao ambayo mume anakaa katika ukoo ao jamaa ya muke wake.

Basi kwa haki inayo fanyika kwa mgeni wa kikundi cha wakaaji wa nafasi, ni haki kweli ya yote yanayo kaa, kila mara isiyoweza pelekwa pengine, sababu imetumiwa bila ruhusa, lakini katika namna nyingine, watoto wa mwenye kufaidika na haki hii wanaweza kuyaridhi. Yafaa kujua kwamba mazoezo zingine, imekatazwa kwa wageni kutumia kiasili.

Yote yanayo patikana katika milki ya msitu ya kundi la wakaaji wa nafasi fulani ni ya kundi hilo tu.

### *II.5. Uwezo Wa Kustarehe Na Milki Za Udongo Za Shirika La Mahali*

Amri ya 2 ya sheria ya tarehe 1 Julai 1885 inasema:

«Hakuna haliye na haki ya kukaa kati bila kibaruwa cha upaji wa udongo ulio huru, wala kuwa nyanganya wakaaji wa asili udongo kunako makao yao: udongo ulio huru unapashwa kuonekana kuwa wa serikali».

Amri ya 2 ya sheria cha tarehe 14 Septemba 1886 kinasema:

«Udongo unao ikaliwa na wakaaji wa asili chini ya uongozi wa sultani wao, itaendelea kumilikiwa na mazoezo na matumizi ya nafasi.»

«Mikataba zilizo fanyika na wakaaji wa asili kwa kupata ao kwa kupangishwa kwa vikundi vya udongo havifanye na serikali na havita andikwa mpaka vinakwisha kukubaliwa na wakili mkuu wa Kongo.»

«Yeye ataweza kujulisha namna na sharti za kufuata kwa masemi ya mwisho ya mkataba huo.»

«Yamekatazwa matendo yote ao mapatano yote yatakayo kuwa na shabaa ya kufukuza wakaaji wa asili katika kata milki ambamo wanaishi ao ya kuwanyima uhuru wao wa kuishi kwa namna ya sawa sawa ao isiyo ya sawa sawa».

Mbele serikali huru ya Kongo liwe, kamati ya majifunzo ya Kongo ya juu, shirika ya inchi zote za Kongo na wasio «wakaaji wa asili» kwa kukaa katika udongo

wa vikundi vya wakaaji wa nafasi, walikua wakichungwa matumizi ya nafasi yaliyo fuatana na mazoezi ya posho; ni kusema madaiwa madeni ya udongo kwa muda.

Amri ya 2 sehemu ya kwanza ya sheria ya tarehe 8 Novemba 1886 inasema:

«Cheti cha kuandika na kinacho maandiko ya yote inayo kuwa imara kinaonyesha ya yote imara mizigo yote, utumwa na sharti ambazo zimeongezwa, kwa kupanwa kwa mwenyeji wa udongo wote uliyo andikwa».

Na amri ya 9 ya sheria moja kinasema kwa ngambo yake:

«Kupanwa kwa vyeti vya kukubaliwa haiondoe kwa wenye kuyafanya kutimiza, katika masikilizano na wakaaji wa asili, matumizi ya nafasi inayo kuwa, yaani ikiwa kwa madeni yanayo julikana kwa jina ya «mazoezo ya posho», hata ikiwa madeni haya hayandikiwe ndani ya vyeti katika mizigo inayo ungwa na mali».

Malipo ya madeni ilijulikana kuwa mapashwa, na kuto kulipwa kwa madeni ina hukumu ya kuvunja ruhusa ya cheti cha kukubaliwa. Kwa neno hilo, mlinda vyeti vya udongo, Nestor Drapier (1902) aliandika:

«Ikiwa kutokana na kuto kulipwa kwa posho, ao mazoezo ya kila siku, magonvi yanatokea kati ya mwenye mali na wakaaji wa asilia, ku vunjua kwa cheti cha kukubaliwa kunaweza kufanyika na vyumba vya waamuzi iki ombwa na mlinda vyeti vya udongo».

«Neno Kukaa katika» inayo tumiwa katika nyaraka iliyo tajwa mbele ilikuwa ivi ivi, kwa ni sababu inaweza kukamatwa kwa maana kubwa ao kwa maana ndogo. Kwa hiyo, kwa namna wana jiingiza katika maana fulani ao fulani, tunafikia kwa majibu mbalimbali kwa hiyo tukikamata mazoezo na matumizi ya nafasi ya vikundi vya wakaaji wa nafasi, inaonekana kwamba kuna udongo mdongo ulio likizo na tukitumia awali ya kitabu cha sheria ya Raisi, udongo ulio huku ina kamata sehemu kubwa saana, udongo unao ikaliwa na vikundi vya wakaaji wa nafasi vinavyo jipunguza kwa vitu vidogo saana.

Inchi huru ya Kongo inapochagua maana nyembamba ya neno «kukaa katika». Kwa hiyo, katika mafundisho ya tarehe 25 Machi 1886 na ya tarehe 20 Agosti 1888 tunasoma kuambatana na maana ambayo serikali inaleta kwa neno «udongo unayo ikaliwa na wakaaji wa asili, tuna pasha kujua kupitia maneno haya, udongo wote ambamo wakaaji wa asili wanaishi, wanalima ao wanatumikisha kwa namna fulani». Katika mafundisho mengine waliongeza:

«Inafaa kulinda kwa wakaaji wa asili pembeni ya kijiji chao hivyo tu udongo kutosha kwao ikiwa ingeli limwa kwa namna ya kawaida; lakini mzunguuko mmoja

kubwa sana waweze kuishi ndani bila kuwa na lazima ya kutenda kufatana na namna zao za mlimo mabadiriko moja isiyo weza kuhakikisha kutimilika tu pole pole saana.»

Mafasirio ya sheria za udongo unayo ikaliwa na wakaaji wa asili itakiwa msingi wa sheria ya tarehe 03 Juni 1906 inayo sema katika amri ya kwanza.

«Ni udongo unao ikaliwa na wakaaji wa asili, kwa ukomo wa mipango zilizo tajwa mbele, udongo ambazo wakaaji wa asili wanaishi, wanalima ao wanatumikisha kwa namna fulani kufatana na zoezi na matumizi ya nafasi. Itafatanishwa kwa wakati ule wa makusudio na wa ma hakikisho inayo julikana na serikali ya umbo na eneo za haki za kukaa kwa wakaaji wa asili. Mwenendo ambamo haki hizi zita kusudiwa na namna zita onekana, utajawa nyuma na liwali mkuu.»

«Mpaka wa udongo itawekwa katika taswira itakayo pelekwa katika chumba cha kulinda cha wakili wa jimbo ndogo yanaweza, kwa kusudi ya kutaka kuendelesha kazi, kutia alama kwa udongo, kwa nukta ya za majulisho, kama vile mipaka, hatari za udongo, miti, maji, kilindi cha maji, barabara, njia, na kadhalika.»

Kukamatwa tena kwa inchi huru ya Kongo na wa Ubeleji haikubadiri sheria ya pori, zaidi kwa yale yanayo angalia udongo na wakaaji wa asili. Katika ripoti za miaka iliyotolewa kwa vyumba, kufuatana na maandiko ya amri ya 37 ya sheria ya tarehe 18 Octoba 1908 ao sheria ya wa koloni, ambamo waliandika juu ya mipaka za pori ya wakaaji wa asili. Kupasua mipaka huko, kulifatanishwa kila mara, sababu ilifwatana na kuwa na watu wa kazi na lazima zenyi kufatika; ni kusema yalikuwa yanafanyika katika vikundi vikubwa vilivyo chaguliwa na wapewaji wa pori. Kwa hivyo basi, kutia mipaka ika achishwa kuwa jumla na yanayo fanyika kufuatana mwendo fulani, yalifanyika tu kufuatana na ombi za eneo.

Kwa kuona bei kubwa za kazi ya kutia mipaka ilionekana bure, kundi la wakaaji wa nafasi wasio heshimu mipaka zilizo tiwa na wanao endelea kutoka inje ya sehemu zilizo achwa kwa ajili yao (udongo unao ikaliwa na udongo wa ao kuongeza, kazi hii ya kuweka mipaka ziliachwa pole pole mpaka zika futika kwa mwaka 1927.

Lakini ukoloni uliomba serikali iendelee kupana eneo ya msitu na sehemu ya eneo kuwapa wenyeji akiba kwa uwenyeji unao wapa amani kwamba hawata sumbuliwa katika kutumikisha haki zao. Ni sheria ya tarehe 31 Mei 1934 inayo leta majibu kwa maulizo yote ya sheria. Kipengele cha 1 cha sheria hii kinasema juu ya awali na kinatafsiri ukomo wa amri kwa maneno haya:

«Kupana kwote ao kupokea kwa milki ya udongo inatanguliwa na uchunguzi fulani itakayo fanyika kwa namna na mwenendo unao ombwa na sheria hii».

«Upekuzi ina shabaa ya kutambua kwamba udongo una ombwa ni huru kwa mgao wa sehemu ao kwa kupewa eneo, na kujua pia umbo na eneo ya haki ambazo wakaaji wa asili wangeweza kuwa nayo juu ya udongo huu…».

Sheria hii ina onyesha kupana kubwa katika mafikiri juu ya udongo wa wakoloni, kwa hiyo, uhuru mapumziko ya udongo hayazaniwe tena. Yanapashwa kwa wakati wote kuelezwa hakika katika kufwatisha maulizo fulani na ombi moja ya mgao wa sehemu ya eneo ao kupewa eneo (ni udongo wa wakaaji wa asili kufuatana na maana ya sheria ya tarehe 03 Juni 1906), sheria hii inavunjwa kwa ukimya mipango ya sheria ya tarehe 03 Juni 1906, inayo angalia kutia mipaka hakika kwa udongo wa wakaaji wa asili.

Mwisho wa maulizo haya unaweza kutoa moja ya mafikiri matatu yafuatayo:

- Ao, udongo uliyo ombwa kwa mgao wa sehemu ao kwa kupanwa eneo ni udongo wa wakaaji wa asili kufuatana na sheria ya tarehe 03 Juni 1906;
- Ao, ni milki ya udongo ambapo wakaaji wa asili wanatumikisha haki zinazo tajwa na amri ya 6 ya sheria ya tarehe 03 Juni 1906, ni kusema, kukata miti za matumizi ya upekee, kuwinda katika milki ya udongo na ya msitu, kuvua katika mito, vilindi, bomo kwa kuheshimu mipaka na kanuni inayo angalia maneno haya, kuchuma matunda na hivyo hivyo…;
- Ao, ni milki ya udongo bila haki ya wakaaji wa asili.

### II.5.1. Wazo la kwanza

Kama kifupi ya upekuzi ina onyesha kama udongo unao tamaniwa na Muombaji ni udongo wa wakaaji wa asili, mipango ilikuwa ina gawanya haki ya kutawaliwa ndani ya haki ya upekee na ndani ya haki ya kundi (ya watu wote).

Amri ya kuishi, kulima ao ya kutumikisha inabaki ya upekee kila siku, kwa kinyume, kila mtu mwenye kuelekewa na kupanwa kwa sehemu ya udongo anapashwa kulipisha malipo mbalimbali yanayo ombwa kama kuna onekana kupotea kwa haki ya kweli na ya upekee.

Kama kijiji kina tawala upana fulani kwa mamlaka ya kiongozi moja fulani, iko makao ya wakaaji wa nafasi. Juu ya kupanwa kwa udongo wakaaji wa nafasi wanapashwa lipwa kwa ajili ya kuleta umasikini kwa asili ya udongo. Malipo ilikua ya kuleta kwa wakaaji vutia wanao simamiwa na mkubwa wa udongo ao kiongozi wa mkusanyiko wa jamaa, anao matumikishi ya udongo na anae husika na mgao wa pesa kwa kila mtu moja kufuatana na asilia yao na zoezi za nafasi.

### II.5.2. Wazo la pili

Kama upekuzi una onyesha kama udongo unaombwa unao faida kwa ajili ya kikundi fulani cha wakaaji wa nafasi ya haki moja zinazo julikana kuwa ya wakaaji, ni lazima kujulisha umbo ya haki hizi: haki ya mawindo, ya uvuvi, ya kuchuma na kadhalika…na upana wa haki hizo. Kwa hilo somo la mwisho inafaa kusikia ugumu wa matumizi wa haki hizo. Kwa kweli, kwa mfano, wakaaji wanaweza juu ya udongo unao onekana kuwa bila mtu, kuchuma kwa muda buyoga, vidudu vyenyi mabawa na mbegu zingine ao mazao maumbile na yaliyo lazima kwa maisha yao. Kwa kupotea kwa haki ya kweli, malipo yanayo ombwa ilikuwa inaletwa kwa mfuko wa uhakimu wa milki ya asili.

### II.5.3. Wazo la tatu

Kama upekuzi una onyesha kama udongo unao ombwa na mwenye kuomba msitu ni milki na haina juu yake haki ya kikundi cha wakaaji wa nafasi, wala haki zingine fulani. Serikali inaweza kufanya mara moja na mwombaji wa udongo mkataba wa kupanwa kwa msitu ao wenye kuongoza mambo ya msitu.

Kwa inayo angalia kununuliwa tena kwa haki ya vitu vyote vilivyo imara na haki ya watu wote, awali ilikua kama bei ya kununua tena, ilipashwa kuwa ya kuenea na ya usawa kufuatana na uwezo wa kununua wa sasa unao pesa.

## *II.6. Sheria Ya Udongo Na Milki Za Udongo Za Shirika La Mahali*

Kufuatana na amri ya 53 ya sheria ya udongo, mtunga sheria alikamata mipangiliyo ifuatayo kwa inayo angalia haki juu ya udongo wa wakaaji wa nafasi:

«Udongo ukaamo vikundi vya wakaaji wa nafasi unakuwa, tangu kuingizwa ndani ya matumizi ya sheria hii, ya udongo wa milki», amri ya 387.

«Udongo ukaamo vikundi vya wakaaji wa nafasi ni huo vikundi vya wakaaji hivyo wakaamo, wanalima ao wanatumikisha kwa namna Fulani kwa upekee ao kikundi kufuatana na mazoezo na matumizi ya nafasi», amri ya 388.

«Haki ya kufurahia iliyo patikana kwa njia sawa juu ya udongo itakanunishwa na sheria ya Raisi wa Jamhuri», amri ya 389.

Inafaa kujua kama ni ya mara ya kwanza kwa mtunga sheria wa Kongo anatumia msemwa «kikundi cha wakaaji wa nafasi», na bila kuyapatia mafasiriyo. Kwa kufunika kosa hilo, mtunga amri wa msitu ata ya fasiria.

Kwa namna ya kukaa juu ya udongo kwa kikundi cha wakaaji wa nafasi, mtunga sheria ya udongo alitishia wazo ndani ya amri ya 1 ya sheria ya tarehe 03 Juni 1906 juu ya udongo wa asilia: «Wanakaa, wanalima na wanatumiksha kwa namna fulani kufuatana na mazoezo».

Kama Raisi wa Jamhuri hakukamata sheria inayo tajwa na amri ya 389, vikundi vya wakaaji wa nafasi wataendelea kutumikisha haki zao za mazoezo juu ya udongo wakaamo, kuondosha tu ndani ya milki inayo amriwa na kukanunishwa.

### *II.7. Misitu Za Asilia Wakati Wa Utawala Wa Wakoloni*

Tangu 1885 mpaka amri 011-2002 ya tarehe 29 Agosti 2002, sheria tano na sheria ya mfalme iliongoza msitu wa Kongo; Kwa sheria hiyo, moja tu ndiyo ina vutia mafunzo hiyo, ni sheria ya tarehe 11 Aprili 1949 juu ya sheria ya msitu ya Kongo-Ubeleji.

Ndani ya sheria hii, kulinganishwa: msitu wa milki, msitu wa asilia, msitu unao kuwa chini ya matumizi ya kamati ya upekee ya Katanga na kamati ya taifa la Kivu na msitu ulio panwa. Misitu zote hizi zilitiwa chini ya sheria ya pori na kuhakimishwa kufuatana na ulio andikwa ndani ya amri.

Amri ya 2 nukta ya 2 inapanga:

«Msitu wa asilia ni kusema viwanja vinavyo funikwa na majani ya gafla ya miti ao ya miti kidogo juu yao kuna julikana haki ya kukaa kwa faida ya wakaaji wa asili kufuatana na namna uhakimu wa mtaa uliona. Mipango ya uhakimu ita onyesha mwenendo wa yote waliyo ona».

Kufuatana na masemi yaliyo onyesha shabaa ya sheria ya tarehe 11 Aprili 1949:

«Ina itwa msitu waasilia, viwanja vinavyo funikwa na mchangano wa gafla wa miti ao wa miti kidogo juu yao kunapatikana haki ya kukaa iliyo pewa wakaaji wa asili kufuatana na matumizi ya amri ya 1 ya sheria ya tarehe 03 Juni 1906». Haki ya kukaa humo msituni ya asili ina ungana sawa sawa.

Kwa kuchunga msitu wa asilia zijulikane kufuatana na amri ya 2 nukta ya 2 cha sheria ya tarehe 11 Aprili 1949, amri ya 2 cha sheria ya bunge no 52-205 kilipanga kama muhakimu mkuu wa kata ao mjumbe wake wata simamisha ndani ya kila sehemu ya pori ya asili penye kufanyika matumizi ya msitu, wazo ya sehemu inayo wezekana kupewa wakaaji wa asili, ya bei ya mazao watakao pewa na mwenyi kutumikisha msitu ndani ya mipaka ya mitaa hii.

Ndani ya milki yao, kamati ya upekee ya Katanga na kamati ya taifa ya Kivu iliyo simamiya kwa matumizi ya msitu wa wakaaji wa asili, amri ya 36. Na mazao ya matumizi ya msitu huo yalikuwa yanapewa wenyeji msitu ao kama haikujulikana itapelekwa kwa mfuko wa uhakimu wa mtaa wa asili ndani ya uhakimu pa patikanapo msitu, ikipunguzwa sehenu iliyo julikana na sheria ya liwali mkuu, sehemu iliyo pewa kwa mfuko wa serikali kwa kamati ya upekee ya Katanga ao kamati ya taifa ya Kivu iliyo badilishwa na matumizi yanayo tokana na matumizi ya msitu huu.

Kufuatana na amri ya 4 ya sheria, msitu wa milki na wa asili ilio gawanywa kwa aina mbili: msitu wa kupangwa na msitu wa kukingwa.

Kwa inayo angalia haki ya kutumia ya wakaaji wa asili, ndani ya msitu wa kupangwa, kuondoa tu zile zilizo julikana na sheria ya kupanga, haki ya mazoezo, haziweze kutumiwa.

Kwa msitu wa kukingwa ulio wa asilia ao ya milki, amri ya 9 na ya 10 ilipanga ifuatayo: «Bila kwenda umbalimbali ya kanuni na mipango inayo angalia haki hizo, wakaaji wa asili wanatumikia haki zao za mazoezi ndani ya msitu wa asili ao milki».

«Matumizi ya uchuluzi kwa wakaaji wa asili, ya mazao ya msitu wenye wana vuna kufatana na mafanyizio ya mazoezi ni huru ndani ya msitu wa kukingwa. Liwali mkuu anaweza kukanunisha ao kukataza mavuno ya mazao fulani ya msitu yenye ataona kama ni ya muhimu kwa uhakiki wa matumizi».

### *II.8. Yanayo Husu Sheria 011-2002 Ya Tarehe 29 Agosti 2002 Juu Ya Sheria Ya Msitu (Code Forestier De 2002)*

Mbele ya kuchambua sheria hii ni ya muhimu kukumbusha matendo mawili ya muhimu kwa usikivu mwema wa sheria hii.

Mbele ya sheria ya udongo, msitu wa Kongo ulikanunishwa na sheria sita:

- Sheria ya tarehe 30 Aprili 1887;
- Sheria ya tarehe 7 Julai 1898;
- Sheria ya tarehe 4 Julai 1912;
- Sheria ya mfalme ya tarehe 30 Mei 1922;
- Sheria ya tarehe 4 Aprili 1934;
- Sheria ya tarehe 11 Aprili 1949.

Sheria hii ya mwisho ilifichuliwa kwa wakaaji kwa miaka 1980, kwani tangu mwaka huo msitu wa Kongo ulitumikishwa kufuatana na mkataba unao itwa

«Garama ya kujisaidia» na «barua ya kusudio» na kwa hiyo, mpaka kubadilishwa mapatano wa mikataba hii ndani ya kupanwa kwa msitu.

Nyaraka mbili ilipata vinyume vya lazima kwa utungo wa sheria ya msitu ya mwaka 2002 mara moja na Sheria no 73-021 ya tarehe 20 Julai 1973 juu ya kanuni kuu ya vitu, ya udongo na ya vitu vilivyo imara na kanuni ya ukingo na kwa njia ya mzunguuko na mipangiliyo ya kurudilia ya katiba ya tarehe 31 Decemba 1971. Kwa kweli, Sheria no 71-008 ya tarehe 31 Decemba 1971 juu ya marudiyo ya katiba ya 1967 ilipanga ndani ya amri ya 1:

«Inaingizwa ndani ya katiba amri moja ya 14 bis inayo andikwa hivi: Udongo na chini ya udongo wa Zaïre kama vile pia mazao yao maumbile ni ya serikali. Sheria inatia sharti na kupanwa kwa muda, ya kurudisha na kurudishiwa ya hiyo. Hata vile, kurudishiwa na kurudisha ikiwa udongo haikupanwa bei, haita omba malipo hata moja.»

Kutumikishwa kwa mpangilio hii ilileta hasara ifuatayo:

- **Udongo:**
  - Sheria no 73-021 ya tarehe 20 Julai 1973 juu ya sheria kuu ya vitu, sharia ya udongo na ya vitu vilivyo weza kuhamishwa na sheria ya ukingo

«Udongo ni mali ya serikali peke yake, isiyo weza kunyanganywa wala kuandikwa», amri ya 53.

- **Chini Ya Udongo:**
  - Sheria ya Raisi 81-013 ya tarehe 2 Aprili 1981 juu ya sheria kuu ya madini na mafuta:

«Kufuatana na mipangiliyo ya katiba, chini ya udongo wa Zaire, ipo na inabaki mali ya taifa na ina: madini, viwanda vya madini, visima vya maji ya kunywa iliyo safi na mafuta», amri ya 1, sehemu ya 1.

- Sheria 007-2002 ya tarehe 11 Julai 2002 juu ya sheria ya madini:

«Mahali panapo maisha ya madini hata mahali panapo mali iliyo undwa, hata maji ya chini ya udongo, hata mahali palipo madini mengi inayo patikana juu ya udongo ao inayo patikana chini ya udongo, ndani ya mito na vijito vya inchi ni mali ya serikali ya upekee yenye haiweze nyanganywa na haiwezi andikwa kwa mkazo», amri ya 3, sehemu ya 1.

- **Mazao Maumbile:**
  - Sheria 82-002 ya tarehe 28 Mei 1982 juu ya kanuni ya mawindo:

«Ulimwengu wa nyama unachanga nyama ya mwitu ya aina zote: inayo mifupa ya mgongo na isiyo na mifupa ya mgongo, nyama ya kunyonyesha, ndege, nyama ya kutambaa chini na aina zingine zote za wanyama wa mwitu, Ulimwengu wa wanyama ya Kongo ni mali ya serikali. Inapatikana ndani ya mali ya asili ya taifa na inapashwa kutumikishwa kwa mafaa ya taifa», amri ya 2.

- Sheria 011-2002 ya tarehe 29 Agosti juu ya sheria ya msitu:

«Msitu upo mali ya asili ya serikali», amri ya 7.

Mkaguo wa katiba ya tarehe 31 Decemba 1971 hai kubishiwa na amri ya 9 cha katiba ya tarehe 18 Februari 2006 inayo panga:

«Serikali inatumia enzi daima sawa vile juu ya udongo na chini ya udongo, juu ya maji na msitu, juu ya eneo la anga, ya vijito, juu ya maziwa kubwa na mito ya Kongo kama vile pia juu ya kijito cha mtaa wa Kongo na juu ya vilima vya bara».

«Namna ya matumikishi na ya kupana milki ya serikali inayo semwa kwa sehemu ya juu ina onyeshwa na sheria».

Sehemu ya 1 ya Kipengele hiki ni moja ya awali kuu katika sheria inayo onyesha mataifa yote. Ona yanayo semwa na Nicolas De Sadeleer kitabu cha msaada (vade-mecum) juu ya sheria inayo angalia mataifa kwa ajili ya yote yanayo maisha nadani-wilaya-Afrika:

«Kwa ajili ya mipango maregevu kati ya inchi ya kaskazini na ya kusini kwa ajili ya kujiwekea vitu vimoja vya elimu ya maisha mbalimbali, kama kwa upekee, uzao wa miji na mimea mbalimbali habari za mali ya kuchangia ya ulimwengu, ikiwa msingi wa uzamini wakati wa maandalizi ya mkutano wa Rio. Na kwa hiyo, habari hii itaachwa na waandishi wa kitabu cha mapatano juu ya umbalimbali ya yote inayoleta maisha kwa faida ya «Shuruli ya moja».

Vile vile, mafikiri ya uhuru daima na wenye utimilifu wa kila inchi juu ya manufaa maumbile ilikamilishwa wakati wa mkutano wa Rio. Katika maongezi ya awali ya pili ya matangazo yanayo sema kwamba «Inchi zina haki huru ya kutumikisha manufaa yao kufuatana na siasa yao ya mazingira na maendeleo», ukurasa 19.

Kwa kifupi, amri ya 9 ya katiba hii haibadili ya tarehe 31 Decemba 1971.

### *II.9. Kujulisha Mahali Ya Shirika Za Wakaaji Mahali Katika Mgao Wa Udongo*

Amri ya 4 ya sheria ya ndani no 08-016 cha tarehe 07 Octoba 2008 kinacho sema juu ya mpangiliyo na matumizi ya sehemu ya udongo ulio chini ya utawala mbalimbali na ulinganifu na serikali. Pia na majimbo inasema:

«Jimbo limegawanyika kwa miji mikuu na wilaya ndogo.»

«Imegawanyika kati ya jimbo:

1. Mji mkuu katika mitaa;
2. Mtaa katika mitaa midogo na/ao katika wilaya zinazo ingizwa ndani;
3. Wilaya ndogo katika mitaa ao kata wala zehebu;
4. Mazehebu katika mikusanyo wa vijiji;
5. Vijiji katika mchango wa vijiji.»

Migao iliyo ya lazima kwa sheria ya udongo ni migao mbili za mwisho ya yote iliyo tajwa mbele.

«Sekta ni jumla ya vikundi vya wakaaji wa asili moja, walio huru, wakiongonzwa na mazoezi. Ya meongozwa na sultani anaye chaguliwa na kupewa mamlaka na serikali. Imehakimiwa kufuatana na mipango ya sheria hii kwa yote, mchango wa vijiji unayo yaunda wana chunga matenengezo yao ya asili (mazoezo yao) kufuatana na mipaka na sharti zilizo katika sheria hii na sheria inayo angalia kazi ya sultani wa asili», amri ya 66.

«Zehebu ya vikoo ni jumla ya vikundi vya asili moja, wanao ongozwa na mazoezo na yameongozwa na sultani anaye chaguliwa kufuatana na mazoezo (asila), anaye julikana na kupewa mamlaka na serikali. Imehakimishwa kufatana na mipango ya sheria na mazoezo isiokuwa umbalimbali na sheria, amani ya watu na tabia nzuri», amri ya 67[1].

---

[1] Matafsiri haya yametoka katika sheria –mipango 081 ya tarehe 2 Julai 1998 inayo angalia matengenezo ya inchi na uhakimu wa Jamhuri ya Kidemokratia ya Kongo.

«Zehebu ya uchaguzi ni mchango ao jumla ya vikundi vya wakaaji wa asili vidogo vidogo, vilivyo huru, vikiongozwa kufuatana na mazoezo, vilivyo na watu wadogo kwa maendeleo yake mazuri, na yakiongozwa na sultani anaye julikana na kupewa mamlaka na serikali. Imehakimiwa kufuatana na mipango ya sheria mpango huu», amri ya 140 sehemu ya 1.

«Zehebu ya vikoo ni jumla ya vikundi vya wakaaji wa asili moja, vikiongozwa kufuatana na mazoezo sultani wa asilia anaye chaguliwa na mazoezo na kupewa mamlaka na serikali….», amri ya 141.

